

[...]

NATHAN Hapo zamani za kale, alikuwapo mtu upande wa mashariki
Aliyepata pete yenye thamani kutoka kwa mkono
Jiwe la pete lilikuwa kito cha mng'aro
Daima iliyong'ara kwazo rangi nyingi sana
Mbali ya hayo, ilikuwa na mema yaliyofichwa ndani yake
Ya kupendwa na Mungu na mtu, ambaye kwa mtazamo huu
Na kwa ushawishi huu, aliivaa. Kwa hiyo

Mtu huyo wa mashariki hakuivuapo pete kidoleni mwake
Na akajitolea kuilinda kwa hali na mali
Daima kwa jamaa yake. Yaani – Kwayo akausia;
Kwanza, kwa mtoto wake wa kiume aliyempenda sana kabisa,
Akamteua kwamba naye aiache hiyo pete
Kwa mwanawe anayempenda zaidi miongoni mwa wanawe – na
Bila kuzingatia uzazi, mtoto mpendwa
Kwa ajili tu ya hiyo pete pekee, lazima daima
Asalie kuwa bwana wa nyumba –
Umenifahamu, ewe Sultani?

SALADIN Nimekufahamu. Endelea!

NATHAN Basi pete ikarithishwa kwa mwana hadi mwana
mpaka kwa baba aliyekuwa na wana watatu;
Wote walio kwake watiifu
Ambao asingeweza jengine zaidi ya kuwapenda wote.
Kuna wakati alionekana huyu, sasa yule, kisha akawa wa tatu.
Kila mmoja akapata upendo wa moyo wake, mwingi wa thamani
Kila mmoja alimwahidi kivyake kuirithi pete hiyo.
Yakaenda hayo kwa muda
Bali punde kifo kikawadia
Na baba huyu mwema akajiona kukereka
Kuwaudhi watoto wawili waloamini ahadi yake
Hilo kamwe asingeliweza
Sasa kipi cha kutenda?
Kwa siri kamuita sonara akamwambia
Kwa mfano wa pete ile -
Afue nyengine mbili.
Na tena kamuamuru asichelee gharama wala maumivu
Kuziunda zifanane ziwe kama ni za kweli
Jambo hilo msanii kalimudu.
Pete hizo zikaletwa, na hata mbele ya macho ya baba
Hakuweza kutambua ipi ile ya asili
Kwa bashasha na furaha anawaita wanawe wote
Kila mmoja kivyake, na kila mmoja kampa

Radhi zake na pete yake, na kisha akafa
Umenisikia Sultani?

SALADIN (ambaye sasa alikuwa amevutiwa naye)
Nakusikia, nakusikia – Malizia kisa chako
Hadi mwisho kifikie – Mbona kitambo hivyo?

NATHAN Kimemalizika,

Kwani yale sasa yafuatayo, yanaweza kukisiwa pasi shaka. –
Mara tu baba alipokwisha kufa, akaja kila mmoja
Na pete yake na kila mmoja kataka
Awe mkubwa wa nyumba yao
Likazuka swali, mzozo, malalamiko. Kwa kila hali; pete halisi haikuwa
Tofauti; -
(baada ya mapumziko ambayo kwayo Nathan akitazamia majibu ya Sultani).
Haikuwa tafauti kabisa, kuliko
sasa ilivyo – kwa imani ya kweli.

SALADIN Vipi? Linakuwaje? Hilo ni jawabu la swali langu?

NATHAN Hapana
Bali laweza kuwa kuniradhi yangu,
Lau siwezi amua baina ya pete hizo,
Baba alizozitaka kwa maelezo yake zifanywe,
Kwamba zisiweze kutofautishwa kati yao.

SALADIN Pete hizo – usinitanie; nilidhani
Dini nilizozitaja kwako
Kutafautishwa zingeliweza
Kama vile kwa mavazi, kwa chakula na kinywaji!

NATHAN Na kwani sivyo hivyo ilivyo kwa msingi wa ushahidi wao
Kwamba zote zimejengwa sawasawa kwenye historia?
Ya mdomo au ya maandishi! – Na
Historia lazima ipokelewe kwa kuaminiwa
Na kwa imani ichukuliwe? Ama sivyo? –
Kwa nani tunaweza kwa urahisi kuweka imani?

Hakika ni kwa watu wetu, ambao ni damu yetu

Na ndani yao tumepata ushahidi wa mapenzi tangu utotoni mwetu
Ambao kamwe hawakutupotosha,
Isipokuwa tulipojiwachia kupotoshwa.
Kwa vipi nisiwaamini wahenga wangu
Kama wewe kwa wa kwako? –
Vipi naweza kukutaka wewe
Kumiliki kile ambacho wazazi wako walikikanusha
Ili kukuleta kwenye njia yangu ya ukweli.
Kama ilivyo kwa Wakristo. Ama sivyo? –

SALADIN (Kwa jina la Mungu aliye hai! Huyu mtu yuko sahihi.

Napaswa kunyamaza.)

NATHAN Sasa turejee kwenye pete zetu
Kama ilivyosemwa, watoto wakalalamika. Kila mmoja kwa jaji
Akiapa kupokea kutoka mkononi mwa baba yake
Pete hiyo moja kwa moja. – Kama ukweli ulivyokuwa!
Baada ya kuwa kapata kwa muda mrefu ahadi ya baba,
Kuna siku angelikuwa na pete hiyo na ndipo akawa nayo.
Baba huyo, kila mmoja akasema, kamwe asingeliweza
Kumpa pete ya kughushi.
Badala ya kumshuku baba kama huyo
Akawa tayari kwa nguvu kuwahukumu kaka zake
Kwamba walikuwa na hatia ya udanganyifu

SALADIN Enhe, kisha na jaji? Nina hamu ya sasa kusikia
Utamfanya jaji aseme nini. Sema!

NATHAN Jaji akasema: ikiwa nyinyi hamumshitaki baba yenu kwangu
Basi sitaweza kutoa hukumu
Je, munadhani ninapaswa kukisia tu?
Au munadhani pete ya kweli itafungua kinywa chake hapa? –
Hebu kwanza ngojeni! Nilisikia pete hiyo ya kweli
Ina nguvu za siri za kumfanya anayevaa
Kupendwa na Mungu na wanaadamu.
Hilo basi liamuwe! Kwani pete za kughushi hazitaweza kufanya hilo! –
Nani kati ya nyinyi kaka wawili wanampenda sana kabisa?
Muko kimya. Je, pete hizi za kufurahisha zafanya kazi ndani tu, si nje?
Je, kila mmoja anajipenda mwenyewe tu?
Nyote ni wadanganyifu mliodangaywa,
Hakuna pete iliyo ya kweli hapa.
Yumkini pete ya kweli imekwenda
Na kwa kutaka kuificha au kuipoteza,
Baba yenu akaagiza tatu kwa moja.

SALADIN La kuchekesha! Jambo la kuchekesha!

NATHAN Na kisha, jaji akaendelea, ikiwa
Mutataka ushauri na sio hukumu yangu
Ushauri wangu ni kwamba lichukueni
Jambo hili kikamilifu kama lilivyo.
Madhali kila mmoja alikabidhiwa pete na baba yake:
Basi kila mmoja na amini kuwa yake ndiyo pete ya kweli. –
Yawezekana baba aliamua kutovumilia tena
Utawala wa pete moja nyumbani mwake! –
Na hakika, kwa kuwa aliwapenda nyote,
Na nyote aliwapenda sawasawa
Isingelimridhisha kumpendelea mmoja,
Kuwa mkandamizaji wa wengine wawili.
Basi kila mmoja apate heshima ya hisia hizi huru. (?)
Pasi na kufungwa kwenye jeuri. Kila mmoja naainuke
Kwa pamoja na nduguze wawili kuonyesha thamani ya pete yake.

Aisaidie nguvu yake kwa huruma, mapenzi, kujitolea
Kwa kujisalimisha ndani ya nafsi yake kwa Mungu,
Na kama thamani ya pete itaendelea
Kujionyesha kwa watoto wa watoto wenu
Baada ya maelfu ya miaka
Basi njooni mbele ya kiti hiki cha hukumu
Juu ya kiti hiki atakaa mtu mwenye busara kuliko mimi
Na ataamua. Nendeni! – Hivyo ndivyo alivyosema
Jaji yule mtukufu.

SALADIN Mungu wangu! Mungu wangu!

NATHAN Saladin,
Ukijiona wewe kuwa ndiye huyu
Mtu mwenye busara aliyeahidiwa:....

SALADIN (ambaye alikuwa ameshika mkono na hakuuondoa mkono wake mpaka mwisho)

Mimi vumbi? Mimi niliye si kitu? O Mungu wangu!

NATHAN Una nini, Sultani?

SALADIN Ewe Nathan, mpendwa Nathan! –
Miaka maelfu kwa maelfu ya jaji wako
Bado haijamalizika. – Kiti cha hukumu si changu. –
Nenda! – Nenda! Lakini uwe rafiki yangu.

Quelle:

Auszug aus *Nathan mwenye Busara* (Nathan der Weise). III, Vers 395-545

Übersetzt von Mohammed Kheled Ghassani unter Mithilfe von Dr. Irmtraud Herms, 2016